UTAFITI WA NGUVUKAZI NA AJIRA YA WATOTO 2000/01

MHUTASARI WA MATOKEO MUHIMU

Utafiti wa Nguvukazi uliofanyika Tanzania Bara mwaka 2000/01 ambao ulitekelezwa na Offisi ya Taifa ya Takwimu kwa niaba ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ulikuwa utafiti mkubwa wa kitaifa ulioshirikisha zaidi ya kaya 11,000; kaya 8,000 za vijijini na zilizobaki za maeneo ya mijini. Utafiti huu ni hatua muhimu ya Wizara katika kuzipa kipao-mbele juhudi za kupambanua na kushughulikia tatizo la ukosefu wa ajira, na hasa baada ya kuanzishwa kwa Sera ya Taifa ya Ajira mwaka 1997.

Leo Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo inatangaza matokeo ya utafiti ambao ulilenga kukusanya taarifa katika maeneo matatu muhimu, ambayo ni; (i) Matabaka ya nguvukazi: idadi ya watu wanaofanya kazi, watu wasio na kazi na wenye kazi zisizotimilifu, (ii) idadi ya watu wanaofanya kazi katika sekta isiyo rasmi, na (iii) Ajira ya Watoto. Matokeo yamechambuliwa kwa mtazamo wa kitaifa na kimataifa.

Walengwa

Utafiti ulilenga watu wote wenye umri wa miaka 5 na kuendelea wanaoishi katika kaya binafsi Tanzania Bara. Jumla ya kaya 11,660 zilihojiwa, kutoka vijiji 100, kukiwa na kaya 80 kutoka kila kijiji na kaya 30 kila eneo kutoka maeneo 122 ya mijini yaliyochaguliwa kutoka katika "National Master Sample"

Utafiti haukuhusisha watu wanaoishi katika taasisi na kaya kwa mfano kambi za jeshi, magereza, hospitali, na zingine kama hizo. Kaya zinazokaliwa na wafanyakazi wa Balozi zilizopo Tanzania pia hazikuhusishwa.

Utafiti ulifanyika kutoka mwezi Aprili 2000 hadi Machi 2001.

Aina ya Taarifa zilizokusanywa

Maswali ya utafiti yalilenga kukusanya taarifa nyingi kutoka kaya na watu wenye umri wa miaka 5 na kuendelea katika maeneo yafuatayo:-

- Kazi za kiuchumi za kaya
- Kazi zisizo za kiuchumi za mtu binafsi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita na siku 7 zilizopita
- Ajira, ukosefu wa ajira na watu wanaofanya kazi ambazo si timilifu
- Kazi zifanywazo na watoto wenye umri wa miaka 5 hadi 17
- Jinsia, umri, elimu na mafunzo ya ujuzi kutoka kwa kila mwanakaya

Mabadiliko ambayo yametokea tangu utafiti wa mwisho kufanyika , mwaka 1990/91

Utafiti wa Nguvukazi 2000/01 ulitumia maswali yaliyotumika katika utafiti uliopita wa 1990/91 ya kupima kiwango cha ajira, ukosefu wa ajira na kazi zisizo timilifu. Pia kwa mara ya kwanza kulikuwa na maswali ya nyongeza kwa ajili ya kupima

viwango hivi kwa mtazamo wa ki-Tanzania. Vile vile yaliongezwa maswali maalum kwa ajili ya kupima kiwango cha ajira ya watoto hapa nchini. Utaratibu huu unawezesha kupima aina na kiwango cha mabadiliko katika vigezo vikuu katika soko la ajira pamoja na kutoa matokeo mapya kwa kuyaangalia kwa mtazamo wa ki-Tanzania. Utafiti umeweza kutoa karibu vigezo vikuu 12 kuonyesha uwezo wa uchumi katika matumizi ya nguvukazi na hali ya soko la ajira.

Vigezo Vikuu vya hali ya Soko la Ajira: Matokeo Makuu

Utafiti wa Nguvukazi 2000/01 umeonyesha kuwa mchango wa Sekta ya Kilimo na Sekta ya Umma katika ajira umepungua wakati ule wa Sekta Binafsi, Rasmi na Isiyo Rasmi, umeongezeka. Pamoja na mabadiliko haya, Kilimo bado kinatoa mchango mkubwa zaidi kuliko sekta nyingine.

Ajira katika Sekta ya Umma imepungua kwa zaidi ya nusu katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Kupungua kwa ukuaji wa ajira katika sekta hii kumesababisha watu wengi kutafuta ajira katika Sekta Binafsi, pamoja na Sekta Isiyo Rasmi. Ajira katika Sekta rasmi ya binafsi imeongezeka kwa zaidi ya mara mbili katika kipindi hiki. Hivyo hivyo ajira katika Sekta Isiyo Rasmi imeongezeka kwa zaidi ya nusu ya kiwango chake mwaka 1990/91, ikionyesha kuwa kaya moja katika kila kaya tatu hujishughulisha na kazi hizi.

Matokeo yanaonyesha pia kiwango cha ukosefu wa ajira nchini kinaongezeka na hasa katika maeneo ya mijini. Kwa jumla ongezeko la ukosefu wa ajira linatokana na kuongezeka kwa tatizo la ukosefu wa ajira mijini.

Tatizo la ukosefu wa ajira linaendelea kuonyesha tofauti ya viwango kati ya wanaume na wanawake wanaoishi mijini, wanawake wakiwa na viwango vya juu zaidi kuliko vya wanaume.

Matokeo kwa kila Kigezo

Kiwango cha ushiriki wa Nguvukazi. Kuna ongezeko la kiasi la ushiriki wa Nguvukazi katika kazi za kiuchumi, kutoka asilimia 72 mwaka 1990/91 hadi 80 mwaka 2000/01. Kikiwa ndio kiwango cha uwingi wa shughuli za kiuchumi katika soko la ajira nchini, kinaonyesha kuwa sehemu kubwa zaidi ya watu wenye umri wa kufanya kazi (miaka 10 na kuendelea) inashiriki katika kazi za kiuchumi kuliko ilivyokuwa miaka kumi iliyopita. Huenda hii imetokana zaidi na kuongeza kwa mara ya kwanza shughuli za kuchota maji na kukusanya kuni kwa matumizi ya kawaida kuwa ni kazi za kiuchumi.

Tofauti kati ya kiwango cha ushiriki wa wanawake na ushiriki wa wanaume katika kazi za kiuchumi imeongezeka. Kiwango cha ushiriki wa wanaume cha asilimia 81 ni alama 8 juu zaidi kikilinganishwa na kiwango cha wanawake, ikilinganishwa na tofauti ya alama 1 tu mwaka 1990/91 wakati kiwango cha ushiriki wa wanaume kilikuwa asilimia 73.

Viwango vya ushiriki katika kazi za kiuchumi vinatofautiana kati ya watu wanaokaa vijijini na wale wanaokaa maeneo ya mijini. Tofauti katika viwango imeongezeka kwa mara mbili, ambapo kiwango cha ushiriki wa watu waishio vijijini kimefikia

asilimia 83; kikiwa ni alama 15 juu zaidi ya kiwango cha mijini, ikilinganishwa na tofauti ya alama 7 mwaka 1990/91 wakati kiwango hicho vijijini kilikuwa asilimia 74.

Asilimia ya watu wote wenye umri wa kufanya kazi ambao wanafanya kazi. Kigezo hiki kinapima uwezo halisi wa matumizi ya Nguvukazi kwa kulinganisha idadi ya watu ambao wanafanya kazi na idadi ya watu wote wenye umri wa kufanya kazi na kuuwelezea uwiano huo kwa asilimia. Matokeo yanaonyesha kumekuwepo na ongezeko la matumizi ya nguvukazi kutoka asilimia 70 mwaka 1990/91 hadi asilimia 76 mwaka 2000/01. Ongezeko hili limesababishwa na watu wa vijijini pekee kwa kuwa uwezo wa matumizi ya nguvukazi mijini ulishaka kutoka asilimia 59.5 mwaka 1990/91 hadi 58.0 mwaka 2000/01. Uwezo wa matumizi ya nguvukazi vijijini uliongezeka kutoka asilimia 72 hadi 81 katika kipindi hiki. Kama ilivyoelezwa chini ya kipimo cha ushiriki wa nguvukazi, sehemu kubwa ya ongezeko hili imetokana na kuongeza kwa mara ya kwanza shughuli za kuchota maji na kuokota kuni kuwa ni kazi za kiuchumi. Shughuli hizi hufanyika zaidi vijijini kuliko mijini.

Aina ya ajira. Mabadiliko katika aina nne za ajira ambazo ni: ajira ya malipo, waajiri pamoja na ajira binafsi (acha kilimo), ajira binafsi katika kilimo na wafanyakazi wa kifamilia wasiolipwa, yanaonyesha kupungua kwa ajira ya malipo na pia ajira binafsi katika kilimo. Ajira ya malipo imepungua kwa asilimia 2 na ajira binafsi katika kilimo kwa asilimia 3. Mwaka 1990/91 mchango wa ajira ya malipo ulikuwa asilimia 9.0 na ajira binafsi katika kilimo asilimia 84. Kwa upande mwingine ajira binafsi (ambayo si kilimo) katika Sekta Isiyo Rasmi na ajira ya kifamilia isiyo ya malipo zimeongezeka.

Ajira ya kisekta. Ajira katika Sekta ya Umma imesinyaa kwa nusu ya kiwango chake miaka kumi iliyopita. Mchango wa ajira Serikalini umeshuka kutoka asilimia 3 hadi 2, pia mchango wa ajira katika Mashirika ya Umma umeshuka kutoka asilimia 2 hadi 0.5. Mchango wa ajira ya Sekta ya Kilimo vile vile umedondoka kutoka asilimia 84 hadi 81. Mabadiliko haya yanaonyesha kuwa vianzio vikuu vya ukuaji wa ajira vinaanza kubadilika na kuhamia kwenye Sekta Binafsi (acha kilimo), rasmi na isiyo rasmi. Mchango wa sekta hizi umeongezeka kutoka asilimia 2.8 hadi 4.5 kwa Sekta rasmi na asimia 8.5 hadi 8.8 kwa sekta isiyo rasmi.

Ajira katika Sekta Isiyo Rasmi. Ajira katika sekta isiyo rasmi imeendelea kukua katika kipindi chote. Matokeo yanaonyesha kuwa kaya moja katika kila kaya tatu zinajishughulisha na kazi kwenye sekta hii, ikilinganishwa na kaya moja katika kila kaya nne mwaka 1990/91. Idadi ya kaya zinazojishughulisha na kazi kwenye sekta isiyo rasmi imeongezeka kwa maeneo yote, vijijini na mijini, ingawa kasi imekuwa kubwa zaidi kwa maeneo ya mijini. Karibu asilimia 61 ya kaya za mijini na zaidi ya robo ya kaya za vijijini zinajishughulisha katika sekta hii ikilinganishwa na viwango vya asilimia 42 na 21 kwa mtiririko huo, mwaka 1990/91.

Kiwango cha ukosefu wa ajira. Kwa kutumia tafsiri ya kimataifa (ILO) ya ajira, kiwango cha ukosefu wa ajira kimefikia asilimia 5.1 ikilinganishwa na asilimia 3.6 mwaka 1990/91. Ongezeko hili limetokana zaidi na ukosefu wa ajira katika maeneo ya mijini kutokana na kuwepo ongezeko dogo kwa maeneo ya vijijini. Kiwango cha ukosefu wa ajira mijini kimeongezeka kutoka asilimia 10.6 hadi 14.8, karibu mara tano zaidi ya ongezeko kwenye maeneo ya vijijini.

Inafahamika kuwa tafsiri ya kimataifa (ILO) inafaa zaidi kutumika kwenye mazingira ya kiuchumi ambapo sehemu kubwa ya watu wanafanya kazi za kudumu- timilifu -za malipo (**regular full-time paid employment**). Kwa kuwa hali sivyo ilivyo Tanzania, ambapo sehemu kubwa, kama si wote, ya watu wanafanya kazi za kujiajiri badala ya kuajiriwa, na kazi nyingi ni za msimu au si timilifu (za ubabaishaji) kwenye ama kilimo au Sekta isiyo rasmi, upimaji wa idadi ya watu ambao wana kazi, watu ambao hawana kazi na watu ambao wapo nje ya nguvukazi kwa kutumia tafsiri ya kimataifa mara nyingi haitoi matokeo yanayotarajiwa. Ni kwa misingi huu tafsiri ya kitaifa ya ajira iliafikiwa ili kuhuisha hali halisi ambayo nguvukazi husika inapambana nayo.

Kwa mujibu wa tafsiri ya kitaifa, kiwango cha jumla cha ukosefu wa ajira ni asilimia 12.9 ya nguvukazi iliyopo nchini. Kiwango cha ukosefu wa ajira mijini ni asilimia 32.0 na vijijini ni asilimia 8.4. Tofauti inajitokeza pia hata ndani ya maeneo ya mijini ambapo katika jiji la Dar es Salaami kiwango cha ukosefu wa ajira ni asilimia 46ikilinganishwa na asilimia 26 kwa maeneo ya miji mingine.

Matokeo yanaonyesha kuwa hakuna tofautu ya viwango vya ukosefu wa ajira kati ya waume na wanawake wanaoishi vijijini, lakini kuna tofauti dhahiri ya viwango kwa watu wanaoishi mijini, wanawake wakionekana kuathirika zaidi kuliko wanaume.

Kiwango cha ukosefu wa ajira kwa Vijana. Vijana wenye umri kati ya miaka 10-34 wanaendelea kuathirika zaidi na tatizo la ukosefu wa ajira kuliko rika lingine kwa kuwa wengi wao hujiunga na nguvukazi kwa mara ya kwanza bila kuwa uzoefu na ujuzi wa kazi. Karibu asilimia 73 ya watu wote ambao hawana ajira ni vijana. Utafiti unaonyesha kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana ni karibu mara nne zaidi (350%) kikilinganishwa na kiwango cha watu wazima na kinakuwa mara mbili zaidi.

Vijana wanaoishi maeneo ya mijini wanaathirika zaidi kuliko wanaoishi vijijini. Kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana kwa rika ni kati ya asilimia 28.4 na 47 mijini ikilinganishwa na asilimia kati ya 8.4 na 11.9 kwa maeneo ya vijijini.

Ukosefu wa ajira kulingana na kiwango cha elimu. Asilimia 47.8 ya watu wote ambao hawana kazi wamehitimu Elimu ya Msingi. Viwango vya ukosefu wa ajira vinatofautiana kulingana na kiwango cha elimu cha mhusika. Wale ambao wana elimu ya Sekondari wana kiwango cha kati ya asilimia 16 na 26, ikilinganishwa na asilimia 14 kwa wale ambao hawakumaliza elimu ya msingi na asilimia 12 kwa wale wote waliobaki. Asilimia 91 ya watu wote ambao hawana kazi hawajapata mafunzo ya aina yoyote.

Ajira kwenye kazi ambazo si timilifu. Kwa misingi ya tafsiri ya kimataifa ambayo ilitumika katika utafiti wa 1990/91, idadi ya watu wanaofanya kazi kwa saa chache kutokana na kukosa kazi ya kutosha muda wote wa kazi (saa 8 kwa siku), na wapo tayari kufanya kazi zaidi, inaongezeka. Kiwango cha ajira kwenye kazi ambazo si timilifu ni asilimia 11.2, ikiwa ni alama 6.9 juu zaidi ya kiwango cha mwaka 1990/91. Katika kipindi hiki idadi ya watu ambao wanafanya kazi pungufu/siyo timilifu imeongezeka kwa kasi kubwa zaidi kwa maeneo ya vijijini, karibu kabisa kuondoa tofauti iliyokuwepo mwaka 1990/91. Kiwango cha ajira ya aina hii ni kikubwa zaidi kwa wanawake wanaoishi mijini kuliko wanaume ingawa tafouti inapungua. Hali ni kinyume kwa maeneo ya vijijini.

Kwa mising ya tafsiri ya taifa ambayo inapima ajira kwenye kazi isiyo timilifu kwa watu ambao ajira ya aina hiyo ni ya kudumu, kiwango cha jumla ni asilimia 5.3 na ni cha juu zaidi kwa wanaume (6.0%) kikilinganishwa na cha wanawake (4.7%)

Kiwango cha watu wenye umri wa kufanya kazi ambao hawana na hawahitaji kazi (nje ya nguvukazi). Kundi ambalo ni muhimu kiuchumi ni idadi ya watu wenye umri kati ya miaka 25 hadi 59 ambao hawana kazi na wala hawahitaji kufanya kazi. Hili ni kundi ambalo kwa kawaida limemaliza shule lakini halijafikia umri wa kustaafu kazi. Utafiti unaonyesha kuwa kuna watu 402,000 kati ya watu 9.6 millioni (au asilimia 4.2) ambao hawana kazi na hawahitaji kufanya kazi wenye umri wa miaka 25-59. Katika hawa, watu 366,000 kati ya 9.0 millioni (au asilimia 4.1) wana umri kati ya miaka 25 na 54, ikilinganishwa na watu 360,000 kati ya 6.4 millioni (au asilimia 5.6) mwaka 1990/91. Mafanikio haya madogo katika kuingiza kundi hili katika shughuli za kiuchumi huenda yametokana na kuongeza kwa mara ya kwanza shughuli za kuchota maji na kutafuta kuni kuwa ni shughuli za kiuchumi.